# SHERIA YA TAASISI YA ELIMU YA ZANZIBAR, 2016
## MPANGILIO WA VIFUNGU

**VIFUNGU** **MAELEZO**

### SEHEMU YA KWANZA
### UTANGULIZI


1. Jina fupi na kuanza Kutumika.
2. Matumizi.
3. Ufafanuzi.


### SEHEMU YA PILI
### KUANZISHWA, NA UONGOZI WA TAASISI


4. Kuanzishwa kwaTaasisi.
5. Kazi za Taasisi.
6. Bodi ya Ushauri.
7. Sifa za Mwenyekiti.
8. Kazi za Bodi.
9. Mwenendo wa Bodi.
10. Uteuzi wa Mkurugenzi.
11. Kazi za Mkurugenzi.
12. Kamati ya Taaluma.
13. Kazi za Kamati ya Taaluma.
14. Uwezo wa Waziri.


### SEHEMU YA TATU
### MASHARTI YA FEDHA


15. Fedha na Rasilimali.
16. Kutumika kwa Sheria ya Fedha za Umma.


### SEHEMU YA NNE
### MASHARTI MENGINEYO


17. Uwezo wa kutunga Kanuni.
18. Vifaa vya kufundishia.
19. Wafanyakazi.
20. Kuhaulishwa mali na madeni.

**JADWELI**

**SHERIA NAMBA 4 YA 2016**
**NIMESAINI**

**{DR. ALI MOHAMED SHEIN}**
**RAIS WA ZANZIBAR NA MWENYEKITI**
**WA BARAZA LA MAPINDUZI**

19th October, 2016

# SHERIA YA KUANZISHA TAASISI YA ELIMU YA ZANZIBAR NA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO

---

**IMETUNGWA** na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.

## SEHEMU YA KWANZA
## UTANGULIZI

Jina fupi na kuanza Kutumika.

**1.** Sheria hii itajulikana kama Sheria ya Taasisi ya Elimu ya Zanzibar, 2016 na itaanza kutumika mara itakapotiwa saini na Rais.

Matumizi.

**2.** Sheria hii itatumika kwa:

(a) Skuli za Serikali na za binafsi; na

(b) Vyuo vya Mafunzo ya Ualimu vya Serikali na Binafsi.

Ufafanuzi.

**3.** Katika Sheria hii, isipokuwa kama maudhui yatahitaji vyenginevyo:

"Bodi" maana yake ni Bodi iliyoanzishwa chini ya kifungu cha ***6*** cha Sheria hii;

"Mwenyekiti" maana yake ni mwenyekiti anayeteuliwa chini ya kifungu cha 6(1)(a) cha Sheria hii;

"Mtaala" maana yake ni mpangilio maalum ambao unahusiana na malengo, mjumuiko wa maelekezo pamoja na njia zinazotumika kama muongozo wa ufundishaji kwa madhumuni ya kufikia malengo yaliyokusudiwa kitaaluma;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Taasisi aliyeteuliwa chini ya kifungu cha 10 cha Sheria hii;

"Taasisi" maana yake ni Taasisi ya Elimu ya Zanzibar iliyoanzishwa chini ya kifungu cha 4(1) cha Sheria hii;

"Vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji" maana yake ni vifaa vinavyotumika katika usomeshaji na kujifunza na inajumuisha vifaa vya maandishi na visivyokuwa vya maandishi na vilivyozingatia watu wenye mahitaji maalum;

"Waziri" maana yake ni Waziri anayehusika na elimu;

"Elimu ya Maandalizi " maana yake ni elimu inayotolewa kwa watoto wa miaka minne hadi mitano kabla ya kujiunga na darasa la kwanza katika Skuli za msingi;

"Rais" maana yake ni Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi;

"Skuli *ya* msingi" maana yake ni Skuli inayotoa elimu ya msingi;

"Skuli *ya* Binafsi" maana yake ni Skuli inayomilikiwa na kuendeshwa na mtu au kikundi cha watu wasiokuwa Serikali;

"Skuli ya Serikali" maana yake ni Skuli yoyote inayoendeshwa na Wizara au taasisi nyengine inayomilikiwa na Serikali;

"Skuli" maana yake ni pahala ambapo elimu rasmi inatolewa;

"Somo" maana yake ni mfumo malumu wa kitaaluma uliopo ndani ya muundo wa mitaala;

"Muhtasari wa masomo" maana yake ni waraka wa ufundishaji ambao unatumiwa na walimu ambao unajumuisha madhumuni, maudhui, ufahamu na taarifa nyengine mahususi kwa masomo.

## SEHEMU YA PILI
## KUANZISHWA, NA UONGOZI WA TAASISI

Kuanzishwa kwaTaasisi.

**4.**-(1) Kunaanzishwa Taasisi itakayojulikana kama Taasisi ya Elimu ya Zanzibar ambayo itakuwa ni Wakala wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

(2) Taasisi itakuwa chini ya ushauri wa Bodi na kusimamiwa na Waziri.

Kazi za Taasisi.

**5.** Kazi za Taasisi zitakuwa ni:

(a) kubuni, kukuza, kufanya mapitio, kurekebisha na kutathmini mitaala kwa ajili ya skuli na vyuo;

(b) kuishauri Serikali kuhusiana na mambo yanayohusiana na ukuzaji na uendelezaji wa mitaala;

(c) kukuza na kufanya mapitio ya viwango, manufaa yaliyopatikana katika kujifunza kutegemea na fani zinazofundishwa katika skuli na kuhakiki kasoro zilizopo kwa mujibu wa ubora wa elimu inayotolewa;

(d) kuandaa na kutathmini vitabu vya rejea, miongozo kwa walimu, mpangilio wa ufundishaji, miongozo maalum ya ufundishaji na miongozo mingine katika kufundisha inayotolewa na wachapishaji mbalimbali na yale ya watu wenye mahitaji maalum;

(e) kueneza maelekezo stahiki ya elimu kwa kuandaa na kuchapisha majarida;

(f) kufanya utafiti na majadiliano kuhusiana na mitaala yanayotoa maelekezo kuhusiana na mambo yanayofaa kufanywa kwa ajili ya upatikanaji wa elimu bora;

(g) kusaidia katika uendelezaji wa malengo ya elimu, sera na vipaumbele vya utaratibu bora wa uendelezaji wa elimu na usimamizi wa taaluma;

(h) kuanzisha mahusiano na Taasisi zinazohusika na uendelezaji na ukuzaji wa mitaala ndani na nje ya Afrika Mashariki;

(i) kuandaa mipango ya kufundisha na kusaidia ufundishaji kwa walimu;

(j) kushauri na kutekeleza Sera ya Taifa kuhusiana na mitaala na uandaaji wa vitabu na visaidizi vyake;

(k) kuweka viwango na kuthibitisha vifaa, zana na vitu vyengine ambavyo vinaweza kutumika kwa madhumuni ya taaluma katika skuli na vyuo;

(l) kutoa huduma na kuwezesha upatikanaji wa vifaa, zana na vitu vyengine kwa ajili ya matumizi katika taaluma;

(m) kushajihisha taasisi za uchapishaji na uandaaji wa machapisho kwa lengo la kusaidia utoaji wa vitabu;

(n) kuchapisha vitabu vya kiada, miongozo ya walimu na vifaa vyengine vinavyohusiana na taaluma;

(o) kuainisha matatizo ya kielimu ndani ya Zanzibar ambayo yanahitaji kufanyiwa utafiti na hatimae kupatiwa ufumbuzi;

(p) kushajiisha na kuweka msingi bora wa uelewa katika mendeleo ya masuala yote yanayohusika na mitaala;

(q) kujihusisha katika uendelezaji na ukuzaji wa mitaala ili kuinua kiwango cha ubora wa elimu;

(r) kutoa vifaa vya kufundishia ili kuimarisha ufundishaji; na

(s) kufanya mambo au kitu chengine muhimu na cha lazima kwa ajili ya, au kinachohusiana na utekelezaji wa kazi zake chini ya Sheria hii au sheria nyengine zinazohusika.

Bodi ya ushauri.

**6.**-(1) Kunaanzishwa Bodi ya Ushauri ya Taasisi ambayo itakuwa na wajumbe wafuatao:

(a) Mwenyekiti ambaye atateuliwa na Rais;

(b) Mkurugenzi wa Taasisi;

(c) Mkaguzi Mkuu wa Elimu;

(d) Mkurugenzi wa Baraza la Mitihani la Zanzibar;

(e) Muwakilishi mmoja kutoka Shirikisho la Watu Wenye Ulemavu Zanzibar;

(f) Wakili wa Serikali kutoka Afisi ya Mwanasheria Mkuu;

(g) Muakilishi mmoja kutoka Jumuiya ya Skuli za Binafsi; na

(h) Muwakilishi mmoja kutoka Jumuiya ya Waajiri Zanzibar.

(2) Mbali ya Wajumbe wanaoingia kwa nafasi zao, wajumbe wengine waliobakia watachaguliwa na Waziri baada ya kushauriana na taasisi husika kwa kuzingatia jinsia pamoja na taaluma zao.

Sifa za Mwenyekiti.

**7.** Mtu atakuwa na sifa za kuteuliwa kuwa Mwenyekiti ikiwa mtu huyo:

(a) ni Mzanzibari;

(b) ana elimu ya angalau Shahada ya Kwanza ya elimu kutoka Chuo kinachotambulika; na

(c) ana uzoefu wa kazi angalau wa kipindi cha miaka kumi katika masuala ya uongozi

Kazi za Bodi.

**8.** Bodi itakuwa na kazi zifuatazo:

(a) kutoa ushauri katika uandaaji wa miongozo na mipango ya Taasisi;

(b) kushauri katika usimamizi na uongozi wa Taasisi;

(c) kushauri juu ya uteuzi wa maafisa wa Taasisi endapo kutakua na haja ya kufanya hivyo;

(d) kushauri juu ya nafasi za kazi za Taasisi;

(e) kushauri juu ya muundo wa chombo cha kushughulikia mitaala ambacho kitaanzishwa na Taasisi;

(f) kushauri juu ya muundo wa Taasisi;

(g) kuthibitisha na kuidhinisha mitaala na vifaa vyengine vya kufundishia na kujifunzia; na

(h) kufanya kazi yoyote iliyopewa kwa mujibu wa Sheria hii.

Mwenendo wa Bodi.

**9.** Masharti kuhusiana na muda wa kutumikia, vikao na mambo mengine yanayohusu mwenendo wa Bodi utakuwa kama ilivyoelezwa katika Jadweli la Sheria hii.

Uteuzi wa Mkurugenzi.

**10.**-(1) Kutakuwa na Mkurugenzi wa Taasisi ambaye atateuliwa na Rais.

(2) Mtu atakuwa na sifa za kuteuliwa kuwa Mkurugenzi ikiwa mtu huyo ni:

(a) Mzanzibari;

(b) ana elimu angalau Shahada ya uzamili katika fani ya elimu kutoka katika Chuo kinachotambulika;

(c) ana uzoefu angalau wa miaka kumi juu ya mambo yanayohusiana na mfumo wa elimu Zanzibar; na

(d) awe na taaluma na uzoefu wa ukuzaji wa mitaala.

(3) Mkurugenzi atakuwa ndiye Mtendaji na msemaji Mkuu wa Taasisi na atakua na jukumu la kusimamia na kutekeleza kazi za kila siku za Taasisi.

Kazi za Mkurugenzi.

**11.**-(1) Mkurugenzi wa Taasisi atakuwa na jukumu la :

(a) kuongoza kazi za Taasisi kwa ufanisi na kuakisi ubora wa huduma;

(b) kushiriki na kuratibu mambo yanayohusiana na mitaala ya elimu kitaifa, kikanda na kimataifa; na

(c) kufanya majukumu mengine yanayohusiana na kazi zilizoainishwa chini ya Sheria hii.

(2) Bila kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Mkurugenzi atawajibika kutekeleza majukumu ambayo ni muhimu na mahususi kwa madhumuni ya:

(a) kutekeleza sera ya taifa ya elimu katika masuala yanayohusiana na maendeleo ya mitaala; na

(b) kuhakikisha utekelezaji wa makubaliano ya kimataifa yaliyokubaliwa na Serikali juu ya masuala ya maendeleo ya mitaala.

Kamati ya Taaluma.

**12.-(1)** Bodi itaunda Kamati ya taaluma kutoka miongoni mwa Wajumbe wa Bodi kwa ajili ya kutekeleza kazi na majukumu kama Bodi itakavyoona inafaa.

(2) Bila ya kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Bodi inaweza kuanzisha Kamati nyengine yoyote kama itakavyoona inafaa kwa ajili ya utekelezaji wa kazi zake chini ya Sheria hii.

(3) Kamati ya taaluma itakayoundwa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, itateua mmoja miongoni mwa wajumbe wake kuwa mwenyekiti wa Kamati.

(4) Kamati ya taaluma inaweza kumualika mtu yeyote ambaye ana maarifa mahususi kushiriki katika vikao vyake kwa ajili ya kutoa ushauri katika jambo lolote linalojadiliwa, lakini mtu huyo hatokuwa na uwezo wa kupiga kura.

(5) Kwa kuzingatia miongozo na maelekezo kama yatakavyotolewa na Bodi, Kamati inaweza kuweka utaratibu wa kuendesha vikao vyake.

(6) Taasisi itatoa huduma za sekretarieti kwa Kamati kutoka miongoni mwa watumishi wake.

Kazi za Kamati ya Taaluma.

**13.** Bila ya kuathiri masharti ya kifungu cha 12 cha Sheria hii, Kamati itakuwa na kazi zifuatazo:

(a) kufanya mapitio ya mitaala ya vifaa vya kujifundishia na kujifunzia kuanzia elimu ya maandalizi hadi vyuo vya ualimu;

(b) kuhakikisha ubora wa programu za kielimu zinazotayarishwa na Taasisi;

(c) kuratibu na kutoa miongozo ya kazi kwa paneli za masomo;

(d) kupitia masuala yote yanayohusiana na mitaala na sera ya elimu na kutoa mapendekezo kwa Bodi;

(e) kupendekeza kwa Bodi juu ya programu za elimu na mitaala iliyotayarishwa au kuthibitishwa kwa kina na taasisi; na

(f) kutekeleza kazi nyengine yoyote watakayopangiwa na Bodi.

Uwezo wa Waziri.

**14.** Waziri anaweza:

(a) kutoa miongozo ya jumla kwa Bodi kuhusiana na utekelezaji wa kazi za Taasisi;

(b) kutoa miongozo mahsusi kwa Bodi kuhusiana na jambo lolote linalohusiana na maendeleo ya mitaala, sera ya taifa ya elimu, au jambo lengine lolote ambalo lina maslahi ya Taasisi au maslahi ya umma.

## SEHEMU YA TATU
## MASHARTI YA FEDHA

Fedha na Rasilimali

**15.** Fedha na rasilimali za Taasisi zitatokana na:

(a) fedha kama zilivyotengwa na kuidhinishwa kwa ajili ya taasisi na Baraza la Wawakilishi;

(b) ada au malipo yatakayolipwa kwa Taasisi;

(c) fedha na rasilimali zitakazopatikana kwa misaada, zawadi, michango, riba au faini;

(d) fedha kwa namna yoyote itakayolipwa au kuwekezwa kwa Taasisi chini ya masharti ya Sheria hii; na

(e) fedha itakayotokana na malipo, kukodi au kuazimisha au iliyotolewa kwa mali iliyowekezwa au iliyopatikana kwa Taasisi.

Kutumika kwa Sheria ya Fedha za Umma.

**16.** Sheria ya Fedha za Umma na sheria nyengine zinazohusiana na fedha za umma zitatumika kwa mambo yote yanayohusiana na Taasisi, ikijumuisha mambo yafuatayo:

(a) makisio ya mwaka ikijumuisha makisio ya ziada;

(b) uwekaji wa vitabu vya hesabu na ufungaji wa hesabu kila mwisho wa mwaka wa fedha;

(c) uandaaji wa maelezo ya fedha;

(d) ukaguzi wa hesabu; na

(e) jambo jengine lolote linalohusiana na fedha za Taasisi.

## SEHEMU YA NNE
## MASHARTI MENGINEYO

Uwezo wa kutunga Kanuni.

**17.**-(1) Waziri anaweza, kwa kushauriana na Bodi, kutunga Kanuni kwa ajili ya utekelezaji mzuri wa masharti ya Sheria hii.

(2) Bila kuathiri masharti ya jumla ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Waziri anaweza kutunga Kanuni mahsusi zinazoelezea:

(a) utaratibu utakaofuatwa katika upitiaji na uandaaji wa mitaala na vifaa vya kufundishia na kujifunzia;

(b) viwango vya vifaa vya kufundishia na kujifunzia na vitendea kazi vinavyotumiwa skuli na vyuo vya ualimu; na

(c) jambo jengine lolote linalohitajika kuelezwa au ni muhimu kwa ajili ya utekelezaji wa Sheria hii.

Vifaa vya kufundishia.

**18.**-(1) Mtu yeyote hatoruhusiwa kutumia au kuuza mihutasari, vitabu vya kiada, au vifaa vya kujifunzia skuli au vyuo vya ualimu mpaka mtu huyo aombe ruhusa ya maandishi na aruhusiwe na Bodi.

(2) Skuli zote za binafsi zitalazimika kutumia mitaala na vitabu vya kiada vilivyothibitishwa na Bodi.

**(3)** Mtu au taasisi yoyote ambaye atakwenda kinyume au kushindwa kutekeleza masharti ya kifungu kidogo cha (1) na cha (2) cha kifungu hiki, itakua ametenda kosa na akitiwa hatiani atalazimika kulipa faini ya fedha za Kitanzania isiyopungua milioni tano au kifungo kisichopungua miaka mitatu au adhabu zote mbili.

Wafanyakazi.

**19.** Wafanyakazi ambao walikuwa wanafanya kazi katika Taasisi ya Elimu kabla ya kuanza kutumika kwa Sheria hii, wataendelea kufanya kazi na kutekeleza majukumu yao katika Taasisi na itatambulika kwamba wameteuliwa au kuajiriwa kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii.

Kuhaulishwa mali na madeni.

**20.** Jambo lolote lililofanywa kabla ya kuanza kutumika kwa Sheria hii, jambo ambalo masharti ya utekelezaji wake yamewekwa chini ya Sheria hii, jambo hilo litaendelea kufanywa au kutekelezwa kama vile limefanywa kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii.

## JADWELI

---

**Utaratibu wa Vikao vya Bodi**
[*Chini ya kifungu cha 9*]

---

Muda wa Bodi.

**1.**-(1) Mwenyekiti wa Bodi atashika muda wa uongozi kwa kipindi cha miaka mitatu kuanzia tarehe ya uteuzi na anaweza kuteuliwa tena kwa kipindi chengine cha awamu moja tu.

(2) Wajumbe wengine wa Bodi, mbali ya Wajumbe wanaoingia kwa nafasi zao, isipokuwa kama uteuzi wao utatenguliwa au kusita, muda wa uongozi utakuwa ni miaka mitatu na wanaweza kuteuliwa tena kwa kipindi cha awamu nyengine moja tu.

Makamu Mwenyekiti.

**2.** Bodi itachagua mjumbe mmoja miongoni mwa wajumbe kuwa Makamu Mwenyekiti.

Vikao vya Bodi.

**3.**-(1) Vikao vya kawaida vya Bodi vitafanyika angalau mara moja kwa kila miezi mitatu na vikao vinaweza kufanyika muda wowote itakapotokea haja kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu yake, kikao kitafanyika katika pahala ambapo Bodi inaweza kuamua kila baada ya muda.

(2) Mwenyekiti ataongoza vikao vyote vya Bodi na endapo Mwenyekiti atakuwa hayupo, Makamu Mwenyekiti ataongoza vikao vya Bodi na endapo Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti hawatokuwepo, Wajumbe waliohudhuria watamteua mjumbe mmoja miongoni mwao kuongoza kikao hicho na Mjumbe atakaeteuliwa atakuwa na uwezo wa kutekeleza majukumu yote ya Mwenyekiti.

(3) Mwenyekiti anaweza kuitisha Mkutano maalum kwa kuzingatia maombi ya kimaandishi yaliyosainiwa na Wajumbe zaidi ya nusu ndani ya siku 21 ya kupokea maombi hayo.

Kusita kuwa mjumbe.

**4.**-(1) Mjumbe wa Bodi atasita muda wake ikiwa itatokea moja ya sababu zifuatazo:

(a) ikiwa atashindwa kutekeleza majukumu ya kazi za Bodi;

(b) ikiwa hatohudhuria vikao vitatu vya Bodi mfululizo bila ya kuwa na sababu ya msingi;

(c) ikiwa amewasilisha barua ya kujiuzulu kwa mamlaka iliyomteua;

(d) kwa mjumbe ambae amekuwa mjumbe kutokana na nafasi yake, atasita kuwa mjumbe wa Bodi ikiwa atasita kuwepo katika nafasi hiyo.

(2) Endapo nafasi ya mjumbe itakuwa wazi kwa mujibu wa masharti ya

kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, mamlaka ya uteuzi inaweza kumteua mtu mwengine kushika nafasi hiyo kwa kipindi kilichobaki.

Akidi ya vikao.

**5.** Zaidi ya nusu ya wajumbe watafanya akidi ya kikao cha Bodi.

Uamuzi wa Bodi.

**6.**-(1) Bodi itafanya maamuzi kwa makubaliano na ikiwa makubaliano hayatafikiwa, maamuzi yatafikiwa kwa wingi wa kura za wajumbe waliohudhuria na kupiga kura na ikiwa kura za wajumbe zitakuwa sawa, Mwenyekiti atakuwa na kura ya uamuzi.

(2) Bila kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, maamuzi yatafanyika kwa kusambaza hati kwa wajumbe na kila mjumbe atawasilisha maoni yake kwa maandishi, ikizingatiwa kwamba Mjumbe anaweza kuitishwa kikao kwa ajili ya kujadili katika kikao cha wajumbe wote na kutoa uamuzi.

(3) Azimio la maamuzi lililowekwa saini na wajumbe wote kwa wakati huo waliokuwepo Zanzibar, lakini wasipungue wajumbe watano na maamuzi hayo yatachukuliwa kama yameamuliwa kwenye kikao halali cha Bodi na yatasainiwa na kuwasilishwa katika kikao cha Bodi kinachofuata.

Kumualika mtu.

**7.** Bodi inaweza kumualika mtu yeyote ambaye si mjumbe wa Bodi kuhudhuria kwenye kikao cha Bodi kama mtaalamu lakini mtu huyo hatokuwa na uwezo wa kupiga kura.

Katibu wa Bodi.

**8.**-(1) Bodi itamteua Mwanasheria wa Taasisi kuwa katibu wa Bodi.

(2) Katibu wa Bodi atakuwa na dhamana ya kunakili na kuhifadhi kumbukumbu za vikao vya Bodi na Kamati.

(3) Kumbukumbu zote za vikao vya Bodi zitathibitishwa na Bodi katika kikao kinachofuata na zitasainiwa na Mwenyekiti na Katibu wa Bodi.

Kutangaza maslahi.

**9.** Mjumbe yeyote ambaye atakuwa na maslahi ama ya moja kwa moja au kinyume chake ya makubaliano yaliyoingiwa na Bodi au yaliyopendekezwa au jambo lolote ambalo linataka kutolewa maamuzi na Bodi, mjumbe huyo atapaswa kutangaza maslahi yake juu ya jambo hilo na hatoruhusiwa kushiriki katika mjadala wa jambo hilo.

Utaratibu wa Vikao.

**10.** Kwa kuzingatia masharti ya Jadweli hii, Bodi itakuwa na uwezo wa kuweka utaratibu mzuri wa kuendesha vikao vyake ikijumuisha vikao vya Kamati za Bodi.

Kamati za Bodi.

**11.**-(1) Bodi inaweza katika kutekeleza kazi zake kuanzisha kamati mbalimbali kama itakavyoona inafaa.

(2) Uendeshaji, masharti na mambo mengine yanayohusiana na Kamati zilizoanzishwa yataainishwa na Bodi.

Posho za Wajumbe.

**12.** Mwenyekiti na wajumbe wengine wa Bodi na Kamati watastahiki kulipwa posho na malipo kwa kiwango ambacho Waziri anaona inafaa kila baada ya muda.

**Umepitishwa** na Baraza la Wawakilishi, tarehe 21 Septemba, 2016.

**[ RAYA ISSA MSELLEM }**
**KATIBU, BARAZA LA WAWAKILISHI**
**ZANZIBAR**